

**Dondoo za Mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam  
19 Septemba 2008**

**Waliohudhuria**

Ally Athuman Jumbe  
Aseli Wilison  
Bashiri Rashidi  
Filbert Mbecha  
Juma Ali Salehe Jongo  
Kassim Bakari  
Kiomani Ally  
Mejah Mbuya  
Mussa Alex  
Nickson Kilunga  
Paulo Atibu Hatibu  
Pendo January  
Rahma Ali  
Shamte J Kigoma

**Wageni**

Eyasu Markus Woldesmyas  
Alphonse Nkurunziza

Mkutano ulianza saa 4.35 (10.35am)

**Kukaribisha Wageni**

Tulianza kwa kuwatambulisha wageni waliokuja kututembelea kutoa Uholonzi - Eyasu Markus Woldesmyas mwanafunzi wa shahada ya uzamili (masters) kutoka Uholonzi lakini rai wa Ethiopia na Alphonse Nkurunziza mwanafunzi wa udaktari wa falsafa ambaye ni rai wa Rwanda.

Wote wapo hapa nchini kwa ajili ya kufanya utafiti kwenye usafiri wa baisikeli hapa nchini hususani jijini Dar es Salaam.

Waliwaeleza wanachama kusudio lao, la wakaomba wanachama waliona muda wagubatane nao kwenye kukagua barabara za jijini kuanzia tarehe 23-26 Septemba 2008. Juma Jongo na Filbert Mbecha walijitolea kuongezana nao. Mejah alijitolea kuwapa baisikeli 2 kwa ajili ya kutumia siku hizo tatu watakazokagua barabara.

Pia waliomba UWABA kupitia wanachama wake wasaidie kujaza dodoso (questionnaires) kuhusu matumizi ya baisikeli ya kila siku ya jiji la Dar es Salaam. Mejah pia alijitolea kutafasiri maswali ya dodoso kwani yalikuwa kwa lugha ya kiingereza.

**Msafara wa Baisikeli**

Mejah, Jongo na Filbert walitoa majibu kuhusu majukumu yaliyopitishwa ya kikao kilichopita kuhisika na msafara wa tarehe 25 Oktoba.

Mbunge wa Ilala, Mhe Zunge amekubali atakuwa mgeni rasmi kwenye msafara kama hatakuwa na majukumu mazito ya kitaifa, lakini kimsingi aliahidi atakuja kwani kalenda yake ilimwonyeshe atakuwa na nafasi siku hiyo. Mejah, Juma na Filbert walikwenda kumwona ofisini kwake Ilala siku ya tarehe 11/09/08.

Bakhresa – Mejah alipiga simu akaongea na Bwana Abdul lakini bado alitushauri tusbiri hadi ufungo wa mwezi utukufu (Ramadhan) utakapokwisha ndiyo atatupa jibu kamili.

Ubalozi wa Ireland – Mpaka kufikia tareheh 19/09/08 bado jibu lilikuwa halijapatikana kutoka ubalozi wa Ireland.

Ubalozi wa China – wamekubali kutupatia baiskeli kama mwaka jana, ingawe bado hatujapata barua ya kiofisi (official letter) kututaarifu ni baiskeli ngapi watatupatia.

CRDB, NMB – simu zote zilizopigwa, hazikutoa jibu la kueleweka, CRDB walidai bajeti ishapita ila waataangilia. NMB walisema tusbiri mpaka wiki ya tarehe 20 na kuendelea ndiyo tujaribu kuwasiliana nao tena.

Tulipata barua kutoka manispaa ya Ilala kuitutaarifu kwamba wamekubali tutumie uwanja wa mnazi mmoja, ingawa cha kushengaza wanhitaji tulipie Tsh 250,000.

### **Warsha ya Cameroon**

Mejah aliwasomea wanachama mambo yaliyotarajiwa kuwasihshwa kwenye warsha ya Cameroon ili kama kuna cha kuongeza au kupunguza. Wanachama wote waliohudhuria waliafiki yaliyokuwa yameandaliwa na mwenyekiti pamoja na katibu.

### **Mambo ya fedha**

Ilipitishwa Juma apewe advance ya miezi 3 ya posho yake ambayo ni Tsh 60,000.

Juma alimpatia mwenye numba advance ya Tsh 40,000 kwa ajili ya mkataba mpya wa pango.

Juma pia alimpatia Mejah Tsh 10,000 kwa ajili ya kupiga simu kufuatilia mambo ya msafara.

Makusanyo ya guta yaliwakihsa pia kwa Juma.

### **Mengineo**

Paulo alishauri tawi la UWABA lifunguliwe Temeke.

Juma na Filbert wataambatane na Alphonse na Yaesu kwenye ukaguzi wa barabara ya Kilwa.

UWABA ilipata mwanachama mpya Shamte Kisoma.

Saa saba na dakika 25 tulifunga mkutano.